



Viwango vya Kilimohai Afrika Mashariki

Uzalishaji wa Mazao



***Imeandaliwa na Shirika la Kilimohai Tanzania- TOAM,
2026***



In cooperation with



Je, naweza kuzalisha mbegu au miche yangu mwenyewe? Na nichague mazao gani?

1

Mbegu na vipando EAOPS 6.1



- Ndiyo, unaweza kuzalisha mbegu au miche yako (vipando, viazi, vitunguu, n.k.) shambani kwako.
- Lazima vikue chini ya kanuni za kilimohai kwa angalau mzunguko mmoja.

- Chagua mazao yanayoendana na mazingira ili kuweza kustahimili magonjwa na wadudu
- Tumia mbegu za kilimohai inapowezekana au za kawaida zisizotibiwa kwa kemikali



Wakulima wanahimizwa kuhifadhi mbegu za asili, kubadilishana mbegu na kulinda bioanuwai na urithi wa kilimo

Wanawake, ambao mara nyingi wana jukumu muhimu katika uchaguzi na uhifadhi wa mbegu, wanapaswa kuungwa mkono kwa kupata fursa sawa ya kupata mbegu bora na mafunzo.

2

Kipindi cha mpito EAOPS 6.3

Nini maana ya kipindi cha mpito na kinachukua muda gani?

Ni muda kuanzia pale mkulima anapoanza kufuata kanuni za kilimohai hadi shamba au mazao yake yanapotambuliwa rasmi kama ya kilimohai. Zingatia:

- Shamba lazima lifuate kanuni za kilimohai kwa angalau mwaka 1 kabla ya kuthibitishwa.
- Kama shamba lilikuwa halitumiki kwa zaidi ya mwaka mmoja halihitaji kipindi cha mpito
- Kama shamba lilikuwa linatumia kemikali nyingi au lina hatari ya uchafuzi, kipindi cha mpito kinaweza kuongezwa kulingana na hali ya shamba

Mazao yaliyovunwa chini ya miezi 36 tangu matumizi ya kemikali hayaruhusiwi kuuzwa kama ya kilimohai

Pembejeo isiyoruhusiwa
imetumika Jan 2022




2022-2024



**Itauza
kama si ya
kilimohai**

Baada ya Jan
2025



**Itauzwa
kama ya
kilimohai**

Mpito



Mwaka 1

**Shamba limekuwa
la kilimohai**

Mbinu za kilimohai
zinatumika

Afya ya udongo ni nini na kwa nini ni muhimu?


Afya ya udongo ni uwezo wa udongo kukuza mazao yenye afya, kuhifadhi maji na kusaidia viumbe hai wa udongoni. Udongo wenye afya huongeza mavuno na kupunguza magonjwa.

Ni mbinu zipi zinazoruhusiwa kutumika katika kuimarisha afya ya udongo?



Ni mbinu zipi
haziruhusiwi
kutumika
katika utunzaji
wa afya ya
udongo?

Katika kilimohai,
utunzaji wa afya ya
udongo unategemea
matumizi ya pembejeo
za asili na njia za
kibaolojia, hivyo baadhi
ya mbinu haziruhusiwi
kwa sababu zinaharibu
viumbe hai wa udongo.



Mbinu kama vile matandazo na mazao funika zinasaidia kupunguza magugu na hivyo kurahisisha kazi hususani kwa wanawake ambao kwa sehemu kubwa wanajihusisha na shughuli za shamba na za nyumbani.

Udhibiti wa wadudu na magugu EAOPS 6.6



Kagua mazao yako mara kwa mara



Lisha udongo kupata mazao yenye afya



Matumizi ya mitego



Matumizi ya uzio kuzuia uchafuzi kutoka mashamba jirani



Kuondoa magugu na mazao yaliyohathirika



Imarisha uwepo wa wadudu rafiki

- Kuua visumbufu kwa kuchoma moto hairuhusiwi, isipokuwa tu katika maeneo maalumu ya uzalishaji baada ya kupata kibali kutoka kwa chombo cha uthibitishaji.
- Matumizi ya bidhaa za GMO au viambata vyake hayaruhusiwi.
- Matumizi ya kemikali sumu hayaruhusiwi.

Hifadhi ya maji: EAOPS 4.2

Tumia maji safi kwa umwagiliaji na usafishaji wa mazao: Epuka kutumia maji yatokayo maeneo yaliyonyunyuziwa kemikali

Uzuiaji wa uchafuzi: EAOPS 4.4

Weka mipaka, vizuizi au maeneo ya kinga (buffer zones) yanayolingana na kiwango cha hatari ili kuzuia uchafuzi wa shamba la kilimohai kutoka maeneo ya jirani.

Utunzaji baada ya mavuno: EAOPS 12

Hifadhi mazao ya kilimohai kwa kutenganisha na tumia mifuko na vifaa visafi.

Utunzaji wa kumbukumbu EAOPS 4.3

Tunza kumbukumbu ya kila unachopanda, namna unavyotunza afya ya udongo, namna unavyodhibiti visumbufu, tarehe ya mavuno, kiasi ulichovuna na kumbukumbu za masoko. Hii itasaidia wakati wa mchakato wa uthibitishaji

Utunzaji wa mazingira EAOPS 4.1

Panda miti na kutunza vyanzo vya maji ili kusaidia kutunza hali ya shamba lako la kilimohai bila kusababisha uchafuzi wa aina yoyote.

Viwango vinahasisha matumizi ya njia zisizo za kemikali katika kudhibiti visumbufu na kurutubisha udongo ili kupunguza hatari za kiafya, hasa kwa wanawake na vijana ambao hushiriki kikamilifu katika shughuli za shambani

Kuhusu kipeperushi hiki

Kipeperushi hiki kinaonesha mahitaji ya msingi ya viwango vya bidhaa za kilimohai vya Afrika Mashariki vijulikanavyo kama East Africa Organic Products Standards (EAOPS). Kiwango hiki kilipitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007 na kufanyiwa maboresho kila baada ya miaka mitano hivyo kuwa kiwango rasmi kwa Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Kipeperushi hiki rahisi kimeandaliwa na Mwamvuli wa Kilimohai Tanzania (Tanzania Organic Agriculture Movement -TOAM) kupitia Mradi wa Kitovu cha Maarifa ya Kilimo Ikolojia Hai Afrika Mashariki (Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology in East Africa – KHEA).

Mradi huu unalenga kuandaa, usambazaji wa maarifa na matumizi ya kilimo Ikolojia hai katika Afrika Mashariki. Unafadhiliwa na GIZ kupitia Biovision African Trust (BvAT)

Unaweza kupata maarifa kama haya na mengine mengi kutoka Tanzania na afrika kwa ujumla kwa kutembelea tovuti: <https://khea-africa.org/> na <https://kcoa-africa.org/>
KHEA Website

Mawasiliano

 info@kilimohai.org

 +255 744 134 999

Machapisho mengine katika mfululizo huu

- Uzalishaji wa Mifugo
- Uchakataji wa Bidhaa za kilimohai
- Uzalishaji wa Viumbe Maji
- Ufugaji wa Nyuki